JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAFUNZO YA VIONGOZI KATIKA NGAZI YA KIJIJI, MTAA NA KITONGOJI

KUONDOA UMASKINI

4

DODOMA
APRILI, 2001

YALIYOMO

Uk.

1. Yaliyomo ii

KUONDOA UMASKINI

1. Utangulizi.....1

2. Mbinu za Kutekeleza Mikakati ya Kuondoa Umaskini.....2

3. Ushiriki wa Wananchi kama Zana Muhimu ya Kuondoa Umaskini 4

4. Vikwazo Katika Kuwawezesha Wananchi Kushiriki Katika Shughuli za Maendeleao.....7

5. Mkakati wa Taifa wa Kuratibu Utekelezaji wa Sera za Kuondoa Umaskini.....8

6. Hitimisho..... 12

KUONDOA UMASKINI

1. UTANGULIZI

Tangu tupate Uhuru Serikali ya Tanzania imetangaza vita dhidi ya umaskini, ujinga na maradhi kwa sababu maadui hawa wanakwamisha maendeleo ya wananchi na kufanya maisha yao yawe duni. Tokea wakati huo, Serikali, kwa kushirikiana na wananchi, imekuwa ikibuni na kutekeleza mikakati na mbinu mbalimbali za kupambana na maadui hawa. Hata hivyo hali ya umaskini imebakia katika kiwango kikubwa Takwimu zinaonyesha kuwa hivi sasa karibu nusu ya Watanzania wote wana kipato ambacho kiko chini ya uwezo wa kuwatimizia mahitaji yao ya msingi kama vile chakula, malazi, mavazi, elimu na matibabu.

Maana ya Umaskini

Umaskini ni hali ya maisha isiyoridhisha. Ni hali ya kuwa na uwezo mdogo wa kumudu maisha. Hali hii inajidhihirisha, pamoja na mambo mengine, kwa kuwa na kipato duni, kuishi katika mazingira duni, kusumbuliwa na magonjwa na ujinga.

Viashiria vya Umaskini

Viashiria vinavyoonyesha hali halisi ya umaskini hapa Tanzania ni kutojua kusoma na kuandika, uhaba wa maji safi na salama, huduma duni za afya, vifo vingi vya wananchi, muda mfupi wa maisha, utapiamlo kwa watoto na watu wazima, uchakavu wa mazingira, ukosefu wa ajira, kipato duni, kutokuwa na mahali pa kuishi au kuwa na makazi duni, na kutofahamu masuala muhimu ya jamii.

Madhara ya Umaskini

Miongoni mwa madhara makubwa ya umaskini ni mmomonyoko wa maadili, ukosefu wa amani na utulivu, afya duni na vifo vingi. Hivyo, wajibu wa Kiongozi wa Serikali katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa ni kutambua madhara haya ya umaskini na kuwa katika mstari wa mbele kuongoza mbinu za kukabili vikwazo vilivyopo ili hatimaye wananchi waweze kuondokana na umaskini.

2. MBINU ZA KUTEKELEZA MIKAKATI YA KUONDOA UMASKINI

Utoaji Huduma za Kiuchumi, Kijamii na Maendeleo ya Wananchi

Utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii hutegemea uwezo wa Serikali ambao nao hutokana na nguvu kazi ya wananchi. Hivyo, kuna umuhimu wa wananchi na Serikali kushirikiana bega kwa bega katika kuimarisha huduma hizo kwa kutekeleza na kudumisha miradi ya maendeleo.

Kwa maana hiyo, uwezo wa Serikali wa kutoa huduma bora kwa kiasi kikubwa unatokana na uwezo wa kifedha ambao wananchi, kwa kodi zao na malipo mengine, wameipa Serikali pamoja na kiwango cha ufanisi wa Serikali yenyewe katika kukusanya na kusimamia mapato na matumizi ya kodi na malipo mengine.

Hatua za Kuondoa Umaskini

Kitovu cha vita dhidi ya umaskini ni kaya. Umaskini na hali duni ya maisha vitaweza kumalizika tu iwapo wananchi wenyewe wataamua kuondokana na hali hiyo kwa kutumia nguvu-kazi iiyopo, rasilimali nyingine zilizopo na misaada kutoka Serikalini au/na sehemu nyingine pale hali

inaporuhusu. Ili kuondoa umaskini, Kiongozi wa Serikali katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa, kwa kushirikiana na wataalam, hana budi kuhakikisha kuwa hatua zifuatazo zinachukuliwa:

(a) Kuelewa hali halisi ya umaskini katika maeneo yao. Anatakiwa kubaini viashiria vya umaskini, na kutumia viashiria hivyo; kuorodhesha kaya ambazo zinabainika kuwa ni maskini;

(b) Kuainisha sababu za umaskini kwa ushirikiano na wananchi katika eneo lake;

(c) Kuhamasisha na kuelimisha kila mwananchi aelewe tatizo la umaskini na ajenge azma ya kuondokana nao;

(d) Kuhamasisha wananchi kutambua fursa zilizopo na uwezo walionao wa kuondokana na umaskini kwa kutumia fursa hizo;

(e) Kujenga na kuboresha uwezo wa ufundi, maarifa na stadi za kazi ndani ya kaya ili kuongeza tija;

(f) Kuchukua hatua za makusudi za kuziwezesha kaya kuunda vikundi vya uzalishaji mali;

(g) Kuimarisha vikundi vya ushirika vya uzalishaji mali na biashara;

(h) Kujenga uwezo wa fedha utokanao na akiba. Bila kujenga utamaduni wa kudunduliza na kuweka akiba, ama kwa mtu binafsi au kwa njia ya ushirika na vyama vya akiba na mikopo au mifuko ya mzunguko, hatuwezi kufuta umaskini;

(i) Kutafuta na kuimarisha masoko kwa ajili ya bidhaa zitokanazo na miradi ya wananchi.

3. USHIRIKI WA WANANCHI KAMA ZANA MUHIMU YA KUONDOA UMASKINI

Maana ya Ushiriki wa Wananchi katika Maendeleo

Ni kuwezesha wananchi kufanya maamuzi ya pamoja kuhusu mipango yao ya maendeleo, utekelezaji wake na ufuatiliaji ili kujua matatizo ya kiutekelezaji na mafanikio yanayopatikana. Maeneo ambayo wananchi wanaweza kushiriki ni kama yafuatayo:-

(a) Kuweka sera, shabaha, malengo na kupanga mikakati na mbinu za kuondoa umaskini;

(b) Kuchangia rasilimali na nyenzo za utekelezaji;

(c) Kutayarisha na kutekeleza mpango au radi wa Kijiji au Mtaa kwa kutumia mbinu za ushiriki;

(d) Kugawana mapato au matunda yatokanayo na shughuli za utekelezaji wa mpango au mradi;

(e) Kufuatilia na kutathmini mpango au mradi;

(f) Kuchangia kwa ukamilifu katika kutoa mawazo katika hatua zote zilizotajwa hapo juu.

Umuhimu wa Wananchi Kushiriki katika Kujiletea Maendeleo

Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Serikali za Vijiji, hapa nchini hazina fedha za kutosha kuziwezesha kutoa huduma bora kwa wananchi wake wote. Kwa hiyo, ubora wa huduma za jamii unategemea sana juhudi za wananchi wenyewe

katika kujiletea maendeleo yao kwa kushiriki kwa ukamilifu katika maamuzi na utekelezaji wa mipango/miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Kwa hiyo, Kiongozi wa Serikali katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa anatakiwa kutambua na kuzingatia kwamba ushiriki wa wananchi katika kuleta maendeleo una manufaa makubwa katika kufikia malengo ya kuondoa umaskini kwa kuhakikisha kuwa nguvu-kazi na rasilimali iliopo inatumika kwa ukamilifu. Manufaa hayo ni pamoja na:

(a) Kumwezesha kiongozi kupata habari na taarifa muhimu zinazotakiwa katika kubuni mipango na miradi inayolenga kuondoa umaskini;

(b) Kuiwezesha serikali Kuu na Serikali za Mitaa kutoa huduma muhimu kwa watu wengi na kwa gharama nafuu kutokana na michango ya nguvu-kazi ya wananchi;

(c) Kuwawezesha wananchi kufikia malengo ya maendeleo kwa haraka na kwa ufanisi zaidi bila migongano wala kulazimishwa;

(d) Kuwawezesha wananchi kujenga misingi ya kujitegemea na maendeleo endelevu.

Hivyo, kinachotakiwa sasa si kulalamika tu, ni kuongeza juhudi na maarifa ya kuzalisha mali na kuwafichua wazembe, wezi, wabadhirifu na watu wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na wakishajulikana wachukuliwe hatua za kisheria bila kusita na bila huruma.

Namna ya Kuwawezesha Wananchi Kushiriki katika Kujiletea Maendeleo

Ili kuwawezesha wananchi kushiriki katika maendeleo, na

hivyo, kuondokana na umaskini, Kiongozi wa Serikali ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa afanye mambo yafuatayo:

(a) Ajenge mazingira na kuweka taratbu nzuri za kuwawezesha wananchi kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za maendeleo. Mazingira haya yanajengwa kwa:

- Kuweka bayana kero na shida za wananchi na kuzipa kipaumbele kwa makubaliano;
- Kuwa na mipango na miradi inayoeleweka vyema na inayolenga kuondoa kero na shida za wananchi katika eneo husika;
- Kujua na kutumia rasilimali zilizopo katika eneo husika;
- Kuwa na sera nzuri za miliki na matumizi ya rasilimali ambazo hazipendelei au kubagua wananchi;
- Kutatua migogoro na mifarakano kwa kutumia haki, busara na hoja na wala si kwa nguvu, upendeleo na uonevu.

(b) Awapatie nafasi na uwezo wananchi kuamua na kusimamia shughuli zao za maendeleo kwa kutumia mbinu zifuatazo:

- Kutumia kamati zilizowekwa kushughulikia masuala mbali mbali ya maendeleo na ustawi wa kijiji, kitongoji au mtaa;
- Kuwezesha utaalam uliopo katika eneo husika kuwafikia wananchi kwa kuwapanga na kuwatumia vizuri wataalam;

- Kujenga na kukuza ushirikiano kati ya uongozi wa kijiji, kitongoji au mtaa na wananchi;
- Kuandaa utaratibu wa mafunzo yanayolenga kuondoa matatizo ya wananchi.

4. VIKWAZO KATIKA KUWAWEZESHA WANANCHI KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA MAENDELEO

Kiongozi wa Serikali ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa hukumbana na vikwazo mbali mbali katika uhamasishaji wa wananchi katika shughuli za maendeleo. Hivyo, ni vema kila kiongozi avielewe vikwazo hivi na namna ya kuvitatua. Vikwazo hivi ni pamoja na:-

(a) Tofauti za Mahitaji na Vipaumbele Miongoni mwa Wananchi

Kiongozi wa Serikali ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa ana jukumu la kubaini tofauti zilizopo miongoni mwa wananchi anaowaongoza na kwa kuzingatia misingi ya ushawishi katika uraghbishi, awe tayari kutumia kila nyenzo zilizopo katika eneo lake la uongozi kurekebisha hali hiyo. Nyenzo hizo ni utaalam, sheria, kanuni, taratibu na mahitaji ya wananchi walio wengi.

(b) Tabia ya Baadhi ya Viongozi kukumbatia Madaraka

Ufumbuzi wa tatizo hili ni kwa kila Kiongozi wa Serikali katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa mwenye tabia hii kuondokana nayo na ahakikishe kwamba anawapatia wananchi anaowaongoza fursa ya kuchangia katika kufanya maamuzi yanayohusu maendeleo yao.

(c) **Upeo Mdogo wa Elimu na Utaalam**

Kila kiongozi wa Serikali ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa abaini utaalam unaopatikana katika eneo lake la uongozi na kuandaa utaratibu wa kuueneza katika jamii nzima.

(d) **Ubadhirifu na Utawala Mbovu**

Ili kuepukana na hali hii, kila kiongozi anatakiwa kuzingatia miiko ya uongozi, kufuata sheria, kanuni na taratibu ili kujenga imani kwa wananchi anaowaongoza.

(e) **Uratibu Mbaya wa Shughuli za Maendeleo Zifanywazo na Taasisi za Serikali na Zisizo za Serikali**

Kila kiongozi wa Serikali ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa anatakiwa kuratibu vizuri shughuli zote za maendeleo. Kiongozi ashughulikie vikwazo vitakavyojitokeza katika eneo lake kwa kushirikiana na Kamati husika.

5. MKAKATI WA TAIFA WA KURATIBU UTEKELEZAJI WA SERA ZA KUONDOA UMASKINI

Lengo la Mkakati wa Taifa wa Kuratibu Utekelezaji wa Sera za kuondoa umaskini ni kutoa Mwongozo wa kupunguza umaskini uliokithiri kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 na hatimaye kuutokomeza kabisa ifikapo mwaka 2025. Lengo hili litafikiwa kwa kufanya yafuatayo:

(a) Kuweka mfumo wa kuratibu utekelezaji wa jitihada za kuondoa umaskini;

(b) Kuweka mazingira yanayowezesha kuondoa umaskini kwa ukamilifu;

(c) Kuwawezesha maskini kushiriki kwa ukamilifu katika miradi ya kuondoa umaskini;

(d) Kuhakikisha kuwa wanawake wanashiriki kwa ukamilifu katika jitihada za kuondoa umaskini;

(e) Kufafanua kwa uwazi mgawanyo wa majukumu na wajibu wa washika dau katika kutekeleza mipango na miradi ya kuondoa umaskini;

(f) Kutoa fursa sawa kwa wanaume na wanawake yakuwawezesha kuishi maisha bora na kuongeza tija. Kwa mujibu wa mkakati huu kila Kiongozi wa Kijiji, Kitongoji na Mtaa, kwa kushirikiana na wataalam, anatakiwa kufanya yafuatayo:

(a) Kuendeleza na kuimarisha misingi ya utawala bora;
kwa mfano, utawala wa sheria, ushirikishwaji wa wananchi, uwajibikaji, uwazi na ukweli.

Sambamba na hayo, kila kiongozi anatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

- Kubuni sheria ndogo za kusaidia utekelezaji wa miradi ya kuondoa umaskini;
- Kuelimisha umma juu ya shughuli za Serikali;
- Kuzingatia masuala ya jinsia katika uongozi;
- Kufanya mapitio na kuratibu sera na maagizo mbalimbali na kuhakikisha

kwamba hakuna migongano katika utekelezaji wake;

- Kubaini maeneo ya mafunzo yanayolenga kuongeza ufaniai wa utendaji kazi.

(b) Kuhamasisha wananchi ili washiriki kwa ukamilifu katika miradi ya kuondoa umaskini kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao;

(c) Kubuni njia za kukuza uchumi wa Kijiji, Kitongoji au Mtaa;

(d) Kuhakikisha kuwa teknolojia sahihi na rahisi inapatikana na kutumika ipasavyo kwa lengo la kuongeza tija;

(e) Kuhimiza matumizi zaidi ya nyenzo za uzalishaji mali kama vile, mboji, samadi na mali ghafi;

(f) Kusimamia mipango ya uzalishaji na uwekaji wa akiba ya chakula cha kutosha kwa kila kaya;

(g) Kuhimiza hifadhi bora ya mazao ili kupunguza upotevu na uharibifu wa mazao;

(h) Kusimamia upimaji wa ardhi katika eneo lake ili kuwezesha wananchi kupata hatimiliki; kusimamia utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kudhitibi uharibifu wa mazingira.

(i) Kubaini maeneo ya kuanzisha viwanda vya kusindika mazao;

(j) Kuhimiza uendelezaji na uanzishaji wa vyama vya ushirika, kwa mfano uchimbaji wa

madini pale yanapopatikana, ujenzi wa nyumba bora, kilimo, ufugaji, akiba na mikopo;

(k) Ujenzi na ukarabati wa miundo-mbinu ya mawasiliano hasa barabara za vijijini na vitongojini;

(l) Kupanua wigo wa mapato na kusimamia vyema matumizi yake katika miradi ya kuondoa umaskini;

(m) Kusimamia mipango ya kupanua, kuboresha na kuchangia elimu shuleni;

(n) Kufufua na kuimarisha Kisomo Chenye Manufaa;

(o) Kusimamia mipango ya upatikanaji wa maji ya kutosha, safi na salama;

(p) Kusimamia mipango ya uboreshaji wa huduma za afya na usafi wa mazingira;

(q) Kubuni mikakati ya kuongeza ajira kwa vijana na kuzuia ajira za watoto;

(r) Kutekeleza Sheria ya Serikali za Mitaa inayohusu mamlaka za wilaya na miji na Sheria ya Nguvu-kazi, ambazo zimempa kiongozi wa Serikali katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa majukumu yafuatayo:

- Kudumisha na kuimarisha amani, utulivu na utawala bora;
- Kushirikiana na Serikali na jamii ili kuboresha na kuendeleza ustawi wa jamii;
- Kuhamasisha wananchi ili waongeze tija;

- Kuandaa mipango ya maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo;
- Kuhakikisha kuwa kila mtu ana nidhamu ya kazi.

Hivyo, kwa mintarafu ya Seria ya Nguvu-kazi Serikali katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa itaunda kamati zitakazohakikisha matumizi sahihi ya nguvu-kazi.

6. HITIMISHO

Ili kuondokana na umaskini kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anapaswa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa. Hivyo, kila Kiongozi wa Serikali ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa hana budi kuhakikisha kwamba kila mtu mwenye nguvu na uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi ipasavyo. Kufanya kazi ni haki na wajibu wa kila mtu mwenye afya njema. Kamwe asiruhusiwe mtu kuzurura ovyo au kutumia muda mwingi katika shughuli ambazo hazina anufaa wala tija kama vile ulevi, kucheza bao na kamari.

Sheria za kudhibiti uvivu na uzururaji zipo. Hivyo, jukumu la kila Kiongozi wa Serikali ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa ni kuhakikisha kuwa sheria hizo zinatumika ipasavyo; na kama hazitoshelezi, sheria ndogo zinaweza kutungwa ili kuhakikisha kuwa rasilimai zilizopo zinatumika kwa ukamilifu kuondoa umaskini. Katika kila ngazi ya jamii, ikiwemo ngazi za kijiji, kitongoji na mtaa wananchi lazima wabebe jukumu la kutathmini hali yao, kutambua hali ya umaskini wao na kero zao na kutambua mahitaji yao muhimu ni nini. **Kisha kama jamii na kupitia taratibu na taasisi zao, kama vile Mkutano wa Kijiji, Mtaa au Halmashauri, waamue nini kiwe kipaumbele chao na ni namna gani wanavyoweza**

kukusanya nguvu zao, ubunifu wao, fedha zao na raslimali zao nyingine katika kuondoa kero zao, kupunguza umaskini wao na kuboresha huduma zao mbalimbali. Mchango wa Serikali ujazie tu pale ambapo uwezo wa wananchi umefikia kikomo chake, au katika kujenga uwezo wa wananchi wa kutekeleza majukumu haya yaliyotajwa. Ikumbukwe daima kuwa **MTAJI WA MASKINI NI NGUVU ZAKE.**